

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dodoma
29 Juni, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kama ifuatavyo:

- 1) Amemteua Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mhe. Mbarouk Salim Mbarouk kuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Jaji Mstaafu Mbarouk ameteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti kwa kipindi cha pili.
- 2) Amemteua Mhe. Balozi Omar Ramadhan Mapuri kuwa Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mhe. Balozi Mapuri ameteuliwa kuwa Mjumbe kwa kipindi cha pili.
- 3) Amemteua Dkt. Zakia Mohamed Abubakar kuwa Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi unaanza tarehe 01 Julai, 2023.

- 4) Amemteua Prof. Idrissa Mshoro kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA). Prof. Mshoro ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi kwa kipindi cha pili.
- 5) Amemteua Bw. Benjamin Mashauri Magai kuwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Kabla ya uteuzi Bw. Magai alikuwa Naibu Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uteuzi huu umeanza tarehe 25 Juni, 2023.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

